

5 : NGUZO YA TANO KUAMINI SIKU YA MWISHO.

Nguzo hii inaingia ndani yake kila ambacho Allah amekieleza yeye na mtume wake (saw), katika yale ambayo yatakuwa baada ya kufa na fitna za kaburi, adhabu za kaburi na neema za kaburi, na yale yatayotokea siku ya kiyama kutoka na vituko vyake na shida za siku hiyo. Na kupita kwenye Swiratwa (njia Maalum), Mizani, Hisabu na malipo, na kugawiwa watu vitabu vya matendo yao baina ya watu, yupo atakae chukua kitabu chake kwa mkono wa kulia, na mwingine atachukua kitabu chake kwa mkono wa kushoto kwa kutokea nyuma ya mgongo.

Kwenye nguzo hii pia kunaingia Imaani ya kuamini kuwa kuna birika (Haudhwi) aliloandaliwa kunywa maji yake Mtume wetu Muhammad (saw), kwani kila Mtume analo birika lake, kama ilivyokuja katika hadithi za mtume (saw), pia katika nguzo hii inaingia Imaani ya kuamini pepo na moto, waumini kumuona Mola wao siku ya Kiyama na kuwasemesha na mengineyo kama ilivyokuja kwenye Quran na Sunnah za Mtume (saw), ni wajibu kuyaamini hayo yote na kuyasadiki katika hali ambayo ameibainisha mwenyezi mungu na Mtume wake.

6 : NGUZO YA SITA NI QADAR.

Na katika nguzo hii kuna kusanyika mambo makuu manne;

1: Jambo la kwanza: Mwenyezi mungu anayajua yaliyotangulia na yatakayokuwa baadae, anazijua hali za waja wake kanzia riziki zao, ajali zao, matendo yao na mengineyo katika mambo yao hakuna kilichojificha kwake Allah (sw).

Allah (sw) anasema:

قال سبحانه: ﴿ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴾ [التوبة: ١١٥].

("Hakika ya mwenyezi Mungu juu ya kila kitu ni mjuzi") (At-Tawbah:115).

2: Jambo la Pili : Kuamini kuwa kila alichokandika mwenyezi mungu amekikadiria na kukidhibiti hukumu yake.

Allah anasema :

قال سبحانه: ﴿ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ ﴾ [يس: ١٢].

(" Hakika kila kitu tumekidhibiti katika kitabu chenye ufafanuzi") (Yasin : 12).

3 : Jambo la Tatu : Kuamini Matakwa yake Allah (Mashiaturun) yaliyotekelezwa tokea zamani, alitakalo mwenyezi mungu linakuwa na asilolitaka haliwi.

Allah anasema :

قال سبحانه: ﴿ كَذَلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴾ [آل عمران: ٤٠].

("Hivyo basi Mwenyezi Mungu anafanya atakavyo") (Al Imran: 40).

4 : Jambo la Nne : Kuamini ya kuwa Mwenyezi mungu ndiye aliyaumba yaliyo kadiriwa kabla ya kutokea.

Allah anasema :

قال سبحانه: ﴿ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴾ [الصافات: ٩٦].

(" Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye waumbeni nyinyi na yale mnayoyatenda") (As-swafat: 96).